# IHOTUBA YA MHESHIMIWA JAPHARY RAPHAEL MICHAEL (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KATIKA OFISI YA RAIS – TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,*

*Toleo la Januari, 2016*

---

## I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2017/18.

2. **Mheshimiwa Spika,**Kwa heshima kubwa naomba kuwashukuru wananchi wote hasa viongozi wangu wa chama wa Jimbo la Moshi Mjini pamoja na viongozi wote wa chama wa Kanda ya Kaskazini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kuhakikisha majukumu yangu ya kuwahudumia wananchi yanatekelezwa.

3. **Mheshimiwa Spika,** Niwashukuru waheshimiwa wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano walionipa katika maandalizi ya hotuba hii, hasa wale wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Aidha, ni mshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wangu Mhe Joseph Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe kwa ushirikiano wake usio na kipimo katika mchakato mzima wa maandalizi ya Hotuba hii.

4. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwa familia yangu kwa uvumilivu mkubwa walionao pale ninapokuwa kwenye shughuli za kichama na za kibunge, nasema natambua upweke wanaokuwa nao kwa mimi kutokuwepo pale ninapohitajika kuwepo.

5. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake,Ibara ya 145 na 146, Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi ambavyo vipo katika ngazi za chini za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vyombo hivi huundwa, huendeshwa, husimamiwa na kuwajibika kwa wananchi wenyewe.

6. **Mheshimiwa Spika**,Katika kipindi kati ya mwaka 1962 na 1972 Serikali za mitaa zilipata mafanikio machache

na matatizo kuwa mengi. Majukumu ya ya halmashauri yaliongezeka kama vile usimamizi wa elimu ya msingi, matibabu, barabara na maji.Uwezo wa halimashauri za miji na wilaya katika kutekeleza majukumu yake ulikuwa mdogo sana kutokana na kuwa na vyanzo vichache vya mapato hivyo kuifanya serikali ione kwamba dhana ya serikali za mitaa haikuwa na tija.

7. **Mheshimiwa Spika,** Mwishoni mwa miaka ya sabini na mwanzoni mwa miaka ya themanini serikali ilirejea dhamira yake ya kuwa na serikali za mitaa zilizo imara ili kutimiza azma ya kupeleka madaraka kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuzipa Mamlaka ya kukusanya mapato kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato.

8. **Mheshimiwa Spika,** Vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa vimeainishwa katika vifungu Na. (6) hadi (9) vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 yaani (The Local Government Finance Act, No. 9 of 1982).Kulingana na Sheria ya Fedha Na. 9 ya mwaka 1982 ya **Serikali za Mitaa** iliyorekebishwa na Sheria ya Fedha Na. 15 ya mwaka 2003 yaani (The Finance Act No. 15 of 2003), Serikali za Mitaa hazitozi kodi ya Mapato. Jukumu hili hufanywa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania yaani (Tanzania Revenue Authorities - TRA) kwa kushirikiana na HAZINA kwa

viwango mbalimbali kwa mujibu wa Sheria na kanuni husika.

## II. UHUSIANO KATI YA SERIKALI ZA MITAA NA SERIKALI KUU

9. **Mheshimiwa Spika,** Serikali Kuu ni **c**hombo ambacho kwa misingi maalum kimepewa mamlaka ya kuendesha utawala wa nchi nzima. Maeneo ya Serikal**i** Kuu yanaanzia Taifa, Mkoa, Wilaya na Tarafa. Serikali za Mitaa ni vyombo madhubuti vya Serikali Kuu katika ujenzi wa utawala bora, demokrasia na kuleta maendeleo nchini. Kufanikiwa kwa Serikali za Mitaa kunategemea zaidi uhusiano na ushirikiano kati yake na Serikali Kuu kwa kujenga mazingira mazuri ya kiutendaji. Ibara ya 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na marekebisho yake inaweka misingi ya uhusiano kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Ili kuwezesha kuwapo na kufanya kazi kwa uhusiano huo, sheria mbalimbali zimetungwa kuhalalisha uhusiano huo. Sheria hizo ni pamoja na:

-

a. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Namba 7 ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na sheria Namba 6 ya mwaka 1999;

**b.** Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Namba 8 ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na sheria Namba 6 ya mwaka 1999;

**c**. Sheria ya Tawala za Mikoa Namba 19 ya mwaka 1997.

Majukumu ya Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa Kwa mujibu wa kifungu cha 174A cha Sheria Namba 7 ya mwaka 1982, na marekebisho ya sheria namba 13 ya mwaka 2006 kifungu cha 54A cha Sheria Namba 8 ya mwaka 1982, majukumu ya Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:

i. Kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu na mamlaka yake kwa kutambua uhuru wake kisheria;

ii. Kubuni na kuweka sera za kitaifa, sheria, kanuni na taratibu kuhusu uendeshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa;

iii. Kutoa ushauri wa kitaalam;

iv. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa sera za kitaifa,sheria, kanuni, taratibu, miongozo na viwango vilivyowekwa kitaifa;

v. Kutoa ruzuku kwa Serikali za Mitaa;

vi. Kuendeleza taaluma;

vii. Kudhibiti mambo ya kisheria na ukaguzi wa fedha na rasilimali za Serikali za Mitaa. Hii inaweza kutekelezwa kwa kutoa mafunzo, kutayarisha taratibu na kanuni mbalimbali na kukusanya takwimu za kitaifa;

viii. Kuweka mazingira yatakayowezesha mamlaka za serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

ix. Kuhakikisha watumishi na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatoa maamuzi na miongozo sahihi wanapotekeleza majukumu yao katika mfumo wa Serikali za Mitaa;

x. Kufanya mambo mengine yatakayowezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria na majukumu mengine kwa ufanisi na kwa kuzingatia sheria.

## III. MADARAKA YA MKUU WA MKOA

**10.** **Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 5 (3) cha sheria ya Tawala za Mikoa Namba 19 ya mwaka 1997 kinaelezea

wajibu wa Mkuu wa Mkoa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa ni kuziwezesha na kuzijengea mazingira ya kutekeleza majukumu yao kisheria. Dhana hii ya uhuru wa mamlaka za Serikali za Mitaa inaegemea katika sharti kuwa, mamlaka hizo zitakuwa zinajiendesha kisheria.

## IV. MADARAKA YA MKUU WA WILAYA

11. **Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tawala za Mikoa Namba 19 ya mwaka 1997, kinampa Mkuu wa Wilaya majukumu ya kuziwezesha na kuzijengea mazingira mazuri mamlaka za Serikali za Mitaa zilizomo ndani ya eneo lake ili ziweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kifungu cha 78A cha sheria namba 8 ya mwaka 1982, kama vile ilivyo kwa Mkuu wa Mkoa, vimetoa uwezo kwa Mkuu wa Wilaya kuchunguza uhalali wa vitendo na maamuzi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika eneo lake.

12. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri Mwenye dhamana kuwaelekeza wakuu wa Mikoa na wakuu wa Wilaya kufanya kazi kwa kuzingatia mipaka yao ya kisheria. Wakuu wa Mikoa na wilaya waepuke kufanya maamuzi yanayorudisha nyuma utekelezaji wa majukumu ya madiwani na watendaji wa halmashauri nchini.

**13.** **Mheshimiwa Spika**, Ni muhimu kuwe na semina elekezi kwa Wakuu wa Mikoa,wakuu wa wilaya,madiwani na watendaji wa halimashauri ili kujua namna bora ya kutekeleza majukumu yao kwa ajili ya kuleta mahusiano mazuri ya kikazi yenye tija na ufanisi Kambi Rasmi ya Upinzani haiamini katika tabia iliyojengeka sasa ya wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kuwanyanyasa watumishi wa halmashauri kinyume cha sheria za Tanzania za utumishi wa Umma.

## V. MABORESHO YA SERIKALI ZA MITAA

**14.** Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa huwawezesha wananchi kuwa na sauti katika maamuzi mbalimbali ama kwa kushiriki moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi wao katika shughuli za maendeleo na utawala. Serikali za Mitaa zinatokana na dhana ya madaraka kwa umma. Dhana na madhumuni ya madaraka kwa umma ni kuwapa wananchi (wanaume na wanawake) wote uwezo na fursa sawa ya kushiriki kikamilifu katika masuala ya siasa, uchumi na utawala katika nchi yao. Kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), wananchi ndiyo msingi wa mamlaka

yote na Serikali inapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.

15. **Mheshimiwa Spika,** Mwaka 1998, Sera ya Taifa ya Uobreshaji wa Serikali za Mitaa **'Policy Paper on Local Government Reform 1998'** iliandaliwa na kuweka bayana umuhimu wa KUGATUA madaraka ya Serikali Kuu kwenda SERIKALI ZA MITAA (decentralisation by devolution au kwa jina lake maarufu D by D ).

16. **Mheshimiwa Spika,** Chini ya Sera hii, Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa (Local Government Reform Programme- LGRP) ilianzishwa kwa dhamira ya kuziimarisha Serikali za Mitaa ili kusukuma mbele utekelezaji wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini yaani Poverty Reduction Strategy na baadaye MKUKUTA, na vile vile kuhakikisha kuwa Halmshauri za Miji na Wilaya zinatoa huduma bora kwa wananchi wake hususan huduma za Afya, Maji, Elimu, na huduma za ughani n.k. (angalia mpango wa "LGRP Medium Term Plan and Budget July 2005 – June 2008" OR – TAMISEMI: Juni 2005 )

17. **Mheshimiwa Spika,** Malengo maalum ya Programu hiyo yalikuwa ni:

i. Kugatua madaraka ya Serikali kuu na kuyapeleka kwenye Serikali za Mitaa (LGAs) ili ziwe na madaraka

kamili (to create more autonomous Local Government Authorities), kupitia 'political decentralisation'

ii. kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kupitia watumishi wa umma wanaowajibika kwa Serikali za Mitaa zenyewe ***('de-linking of local authority staff from the respective line-ministries, making them accountable to the LGA who will be their employer, fully responsible for all human resource management'- Administrative Decentralisation)***

iii. Kuziwezesha Halmashauri kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake na kuwa na mfumo wa mgawanyo wa mapato kati ya Serikali kuu na Serikali za Mitaa (financial decentralisation)

iv. Kwa umuhimu wa kipekee maboresha pia yalikuwa na dhamira kuu ya kubadilisha mfumo wa mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kutoka mfumo wa Serikali Kuu wa kuwa na ***'control role'*** na hivyo kuwa na wajibu wa kutunga sera na kuweka vigezo vya ubora wa huduma; na kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza sera kwa kuwajengea uwezo na kuwapatia raslimali fedha na utaalamu ili ziweze kutoa huduma inayolingana na ubora uliowekwa na kukubalika.

**18. Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe kuwa, Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ilitekelezwa sambamba na programmu nyingine za uboreshaji wa Sekta za Umma na Sekta Binafsi. Moja kati ya nyanja muhimu za uboreshaji wa Sekta ya Umma ni uboreshaji wa Utumishi wa Umma yaani Civil Service Reform Programme (CSRP 1998), ambayo baadaye iliboreshwa na kutengeneza programu maalum ya miaka kumi na mitano Public Service Reform Programme (2000 -2015) yenye malengo makuu yafuatayo:

i. Kuboresha utendaji
ii. Kuweka tabia ya kufuatilia, kupima na kutathmini utendaji katika utumishi wa umma na utoaji wa huduma za umma
iii. Kuweka mifumo ya kuinua kiwango cha ubora wa huduma (quility improvement cycles).

**19. Mheshimiwa Spika,** Maboresho hayo yalidhamiria kuimarisha utawala na utoaji huduma. mambo ambayo ni muhimu sana katika kuiondoa nchi yetu kwenye umasikini na pia kufikia vigezo vya mpango wa Maendeleo ya Millenia wa kupunguza umasikini wa kipato na nchi yetu kuwa na uchumi wa kati.

**20. Mheshimiwa Spika,** Awamu za kwanza za Maboresho hayo ya Serikali ya Mitaa yalichukua miaka

kumi, kuanzia mwaka 1998 -2008, katika kadhia hiyo sera ya D by D (Decentralizion by Devolution) ndiyo ilipata umaarufu sana. Kwa masikitiko makubwa ni kwamba uwekezaji wote huo uliofanywa na Serikali za awamu ya tatu na awamu ya nne umekuwa ni kazi bure, kwa vile katika uhalisia madaraka yamerudishwa Serikali Kuu.

**21.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya awamu ya tano ambayo wananchi walikuwa na matumaini makubwa kwayo katika kugatua madaraka kwa lengo kukuza Demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi katika mipango yao ya maendeleo na utawala bora inafanya kinyume kabisa na matarajio ya wananchi.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini ugatuaji wa madaraka ni jambo la msingi sana katika kuleta ustawi wa maendeleo ya watu hivyo inaishauri serikali ya awamu ya tano isimamie na kutekeleza dhana ya ugatuaji wa madaraka kwa vitendo.

## VI. HALMASHAURI KUKOSA MAMLAKA KAMILI YANAYOLINGANA NA DHAMIRA HALISI YA KUANZISHWA SERIKALI ZA MITAA

**22.** **Mheshimiwa Spika,** Ni ukweli kwamba Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa ndio msimamizi mkuu wa Serikali za Mitaa. Kwa njia hii

Serikali za Mitaa zinawajibika moja kwa moja kwa wizara hii kwa chochote kile kinachofanywa na Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji.

Kwa lolote lile Waziri Mwenye dhamana anaweza kuamua kuivunja halmashauri ya wilaya,manispaa au jiji na kuteua Tume ya kusimamia uendeshaji wa halmashauri ya wilaya, manispaa au jiji husika. Aidha, waziri ana mamlaka ya kumhamisha au kumsimamisha kazi mtendaji mkuu au Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mfumo mzima wa kuwawajibisha viongozi wa kisiasa katika ngazi za halmashauri nao unaingiliwa sana na maamuzi ya Serikali kuu. Mambo haya yote kwa ujumla wake ndiyo yanaondoa Mamlaka kamili ("autonomy") ya Serikali za Mitaa na kufanya maboresho ya miaka kumi na sera nzima ya D by D kuwa ni bure na ni hasara kwa walipa kodi wa Tanzania.

**23.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ni kuwa na uwezo wa kuajiri na kufukuza (hire and fire) kukosa mamlaka hayo maana yake ni kiini macho cha Mamlaka hivyo basi Serikali za mitaa sio Serikali kamili kama inavyotamkwa ndani ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977.

**24.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali za Mitaa zilikuwa na sheria yake ya kuwa na uwezo wa kuajiri na kufukuza

watumishi wake***(hire and fire) ambayo*** ni sheria namba 10 ya mwaka 1982 (The Local Government Servise Act, No.10 of 1982), Lakini Serikali kuu kwa kufikiri kuwa Halmashauri zitakuwa na nguvu za kuweza kuwatumikia watanzania kwa kiwango cha juu na kuweza kuwaondolea umasikini, mwaka 2002 iliifuta sheria hiyo na kutunga sheria ya Utumishi wa Umma namba 8 (The Public Service Act. No.8 of 2002. Sheria hii ilipoka madaraka ya Halmashauri kuhusu utumishi na kurejesha madaraka hayo chini ya Ofisi ya Rais.

**25. Mheshimiwa Spika**, Kuzipunguzia mamlaka halmashauri ya kusimamia watumishi wake hasa Mkurugenzi na Wakuu wa Idara kunasababisha ubunifu wa watumishi wa halmashauri kuwa wa chini sana kwa vile wamekuwa wakiendesha halmashauri kwa mipango ama ya zimamoto au maagizo na miongozo kutoka ngazi ya Serikali Kuu, bila kujali hali halisi ndani ya halmashauri zao.

Aidha, nidhamu ya Wakurugenzi na watumishi wa halimashauri kwa Madiwani ambao ndio wenye halmashauri kwa niaba ya wananchi imekuwa ya chini mno hivyo kufanya maagizo mengi ya mabaraza ya madiwani katika halmashauri kutotekelezwa kwa kuwa Wakurugenzi na manejimenti za halmashauri wanaweza wakaamua kupuuza maagizo hayo.

**26.** **Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya wakuu wa Mikoa na wakuu wa Wilaya wamekuwa tena sio washauri na waangalizi wa mienendo ya utendaji wa halmashauri bali wamekuwa wafanya maazimio ya shughuli za kila siku za halmashauri badala kuheshimu maazimio ya vikao vya kisheria vya halmashauri zetu.

**27.** **Mheshimiwa Spika,** Na kwa vile wao wana kofia ya kumwakilisha Mh Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamekuwa wakitumia mamlaka yao kuwalazimisha Wakurugenzi kutekeleza maagizo yao na kupuuza maazimio ya Baraza la Madiwani, jambo ambalo limekuwa likileta mivutano mikubwa kati ya madiwani na wakurugenzi katika halmashauri hapa nchini hivyo kudumaza maendeleo ya watu wetu.

**28.** **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri serikali kuangalia upya sheria hii ya utumishi na ajira katika serikali za mitaa ili kuwe na utaratibu wa ajira za Wakurugenzi na wakuu wa idara ambao mchakato wake utaanzia kwenye vikao vya kisheria vya halmashauri hata kama itakuwa ni kutoa mapendekezo kwa Waziri mwenye dhamana kwa watu wenye sifa watakaokuwa wameomba ajira hizo za ukurugenzi na ukuu wa idara ili waziri ateue kutokana na mapendekezo ya halmashauri husika.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba kwa kuzipa Mamlaka Halmashauri kutoa mapendekezo ya ajira za Wakurugenzi na wakuu wa Idara kutaleta nidhamu ya uwajibikaji katika halmashauri nchini.

VII. UWEZO WA HALIMSHAURI KUKOPA AU KUINGIA UBIA NA SEKTA BINAFSI-PRIVATE PUBLIC PARTINERSHIP(PPP)

**29.** **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya fedha ya Serikali za mitaa ya mwaka 1982 inaziruhusu halmashauri kukopa katika taasisi za fedha ili kuwekeza katika miradi ya maendeleo.

Jambo la kusikitisha nI pale ambapo Waziri mwenye dhamana anapoamua kuinyima kwa makusudi kibali cha kukopa halmashauri ambayo imetimiza vigezo vyote vya kukopa katika taasisi za fedha ili kuwekeza katika miradi ya maendeleo ambayo inajiendesha yenyewe kwa faida.

**30.** **Mheshimiwa Spika**, Kuna kila dalili kwamba kuna ubaguzi wa kisiasa unaofanywa ama na Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI au Serikali nzima ya awamu ya tano kwa kuzibagua Halimashauri zinazoongozwa na vyama vya upinzani kama vile za jiji la Arusha, jiji la Mbeya, Manispaa ya Iringa, Manispaa ya MoshI, n.k ili kuzifanya zishindwe kutimiza wajibu wake wa kuwaletea wananchi maendeleo na

hatimaye wananchi wapoteze imani na vyama vya upinzani.

31. **Mheshimiwa Spika,** Mfano mzuri ni uamuzi wa Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI kuamua kwa makusudi ama kuchelewesha au kukataa kutoa kibali cha kukopa kwa Manispaa ya Moshi kwa mradi wa ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi yaendayo mikoani (modern Terminal Bus Stand) ambapo Benki ya Rasilimali ya Tanzania (TIB) iko tayari kuwekeza kwenye mradi huo kwa kutoa zaidi ya bilioni ishirini kwa mfumo wa 'Design Build, Operate and Transfer' (BOT). Mradi huo ambao kuufanyia upembuzi na uchambuzi yakinifu umetumia takribani milioni mia Tatu fedha ya walipa kodi na ikathibitika kwamba ni wa faida kiuchumi unanyimwa kibali ili kuwakomoa wananchi wa Manispaa ya Moshi.

32. **Mheshimiwa Spika**, Imani ya kwamba kuna kila dalili ya ubaguzi wa kisiasa unaofanywa na ama na waziri mwenye dhamana na TAMISEMI au na Serikali kwa ujumla wake ni kutokana na Waziri huyo huyo kutoa kibali cha miradi ya aina hyo kwa manispaa ya Morogoro na jiji la Tanga. Huo nI upendeleo mbaya sana na matumizi mabaya ya madaraka (double

standards) yanayofanywa na Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI.

33. **Mheshimiwa Spika**, Ni ukweli kwamba Karibu miji yote ambayo inaongoza kwa kuwa walipakodi wazuri na hivyo kuchangia vyema katika pato la Taifa, kwa mujibu wa taarifa za Benki Kuu, miji hiyo inaongozwa na vyama tofauti na chama Tawala, na miji hiyo ukiondoa jiji la mwanza( GDP 4.09 trilioni) ipo katika mikoa ya Dar ess Salaam (GDP 7.5 trilion), Mbeya (GDP3.2 trilion), Arusha (GDP 2.1 trilion), Tanga (GDP 2.09 trilion), na Kilimanjaro (GDP 2.03 trilion)

Hivyo kwa msingi huo, sio sahihi kabisa kuibagua miji hiyo katika kuigawia keki ya Taifa hasa pale wawakilishi wa wananchi wanapotaka kutumia fursa za kiuchumi walizo nazo ili waharakishe maendeleo ya watu wao.

34. **Mheshimiwa Spika**, Serikali lazima itambue kwamba ina wajibu wa kuwatumikia wananchi wote bila ubaguzi wowote kwa vile watanzania wote kwa namna moja ama nyingine wanalipa kodi hivyo serikali kuwapelekea maendeleo sio hisani bali ni wajibu.

Aidha, uamuzi wa uchaguzi wa viongozi wanaowakilisha wananchi ni wa kIkatiba ambao tumejipangia wenyewe kama Taifa. Hivyo wananchi wasiadhibiwe kwa vile wamechagua wawakilishi

kupitia vyama vya upinzani kwa kuwa wamefanya uamuzi halali wa kikatiba

35. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kurejea kwenye adhima yake ya maboresho ya Serikali za Mitaa ili kuzifanya halimashauri zijitegemee kwa kiwango kisichopungua asilimia 35 kwa kubuni mIradi ya uwekezaji na kutafuta vyanzo vipya vya mapato vIsivyo na kero kwa wananchi. Pia Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI awatumikie watanzania wote bila ubaguzi wa kisiasa wala kikanda.

36. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba chanzo kikubwa cha matatizo ya mapato yanazozikabili halmashauri zote kwa ujumla ni kutokana na udhibiti unaofanywa na Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa. Hivyo basi ili kurekebisha kasoro hizo ni kuifanyia marejeo sheria za fedha hasa kifungu cha 60 kinachohusu halimashauri kukopa, na kuondoa sharti la ridhaa ya ya Waziri mwenye dhamana ili halmashauri ziweze kukopa kwenye taasisi mbali mbali za fedha

## VIII. JUKUMU LA UTOAJI HUDUMA ZA JAMII KATIKA MANISPAA NA MAJIJI

**37.** **Mheshimiwa Spika,** Manispaa na majiji makubwa Duniani yanakabiliwa na Changamoto za kuongezeka kwa wakaazi wake,jambo hilo limesababisha uwepo wa mahitaji makubwa ya huduma za kijamii na za kiuchumi kama vile Afya,Elimu, Maji, Huduma za uokozi,Usalama wa raia na Huduma za usafiri.

**38.** **Mheshimiwa Spika**, Baada ya kupitia nyaraka mbali mbali zinazosimamia kazi zinazofanywa na Mameya wa Manispaa na majiji mbali mbali Duniani kuhusiana na utoaji wa Huduma za kijamii na za kiuchumi kwa wakazi wa Majiji na Manispaa imeonekana kwamba Mameya na Kamati zao ndio wenye Mamlaka ya mwisho ya kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo ihusuyo manispaa zao na majiji yao ikiwemo wao kuwa maafisa masuhuli na watendaji wakuu (accounting officer and executive mayors ) wa Manispaa zao na majiji yao.

**39.** **Mheshimiwa Spika**, Dhamira ya Kambi rasimi ya upinzani kwenye hoja hii ni kuishauri serikali namna bora ya kusimamia huduma ya usafiri katika majiji hususani usafiri wa Umma, UendeshajI wake na miundo mbinu yake kama mabasi madogo na makubwa ya mwendo kasi,tax,Pikipiki, Treni na vivuko katika majiji husika ndani ya nchi ya Tanzania.

lengo kuu likiwa ni kuangalia namna ambavyo sheria namba 8 ya mwaka 1982 inayounda mamlaka za miji,Manispaa na Majiji inavyoweza kufanyiwa marekebisho ili uendeshajI na umiliki wa miundombinu ya usafirishaji wa abiria,matengenezo na ukarabati wa miundombinu yawe jukumu la msingi la uongozi wa Majiji

**40. Mheshimiwa Spika**, Majiji yaliyoangaliwa kama ya mfano ni;

1) Jiji la London ambalo limeanza mamlaka inayoitwa 'Great London Authority'ambayo ipo chini ya Meya wa London na ina jukumu la kusimamia Mfumo mzima wa usafiri wa jiji la London.

2) Jiji la Cape Town ambalo jukumula usafiri wa abiria lipo chini ya Ofisi ya Meya ambapo kimeanzishwa chambo kinachoitwa Transport for Cape Town(TCT)ambacho kinaendesha mrdI unaitwa 'MyCITY bus service'.Chombo hiki kina mamlaka ya ya kupanga,kusimamia na kuratibu shughuli zote za usafiri katika jiji la Cape Town ikiwa ni Pamoja kutengeneza na kukarabati miundo mbinu ya usafiri yaani planning costing,contracting,regulating,monitoring,evaluating,c ommunicating,managing, and maintaining the city of Cape Town's Transport infrastructure, systems,operation ,facilities and network'.

3) Jiji la Johannesburg ambalo waliunda chombo kinachoitwa Rea VAYA chenye maana ya the City of Johannesburg’s revolutionary Bus Rapid Transit System kikiwa na lengo la kutoa usafiri wa haraka,salama na unaohimlika kwa Wananchi yaani ‘Offering fast, safe and affordable public transport on a network of bus routes across Johannesburg’

**41. Mheshimiwa Spika,** imetulazimu kuonyesha jinsi majiji makubwa yanavyotoa huduma kwa wananchi wake na jinsi Ofisi za Meya na kamatI zao zinavyofanya kazi.

**42. Mheshimiwa Spika**, kwa Muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kitendo cha serikali kuingia mikataba ya mikopo kwa ajili ya jiji la Dar es salaam ili Kujenga miundo mbinu ya usafiri ni kuifedhesha hadhi na nguvu ya Meya wa jiji lakini pia ni kuibebesha mizigo mikubwa serikali kuu kwa majukumu ambayo ni ya Halimashauri ya jiji la Dar es salaam chini ya Meya wa jiji na Mameya wenzake wa manispaa za Dar es salaam ambapo serikali kuu ingekuwa mdhamini tu(Guaranter).

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaendelea kuishauri serikali kuona namna ya kufanya marejeo ya sheria namba 8 ya mwaka 1982 ili iweze kuwafanya Mameya wa Manispaa na majiji wawe Mameya watendaji (executive Mayors) wenye Mamlaka kamili na

ikiwezekana sheria itamke kwamba watapigiwa kura na wananchi wote wa eneo husika ili wawe na wigo mpana wa kuwahudumia wananchi wote kwenye maeneo yao ya utawala.

## IX. MUINGILIANO WA MAAGIZO NA MAELEKEZO KATIKA HALIMASHAURI

**43. Mheshimiwa Spika,** Katika muendelezo huo wa kupoka madaraka ya Serikali za Mitaa, katika marekebisho ya sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa ya mwaka 2006, inaonesha kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri ambao ni wateule wa Serikali Kuu wanalazimika kupeleka taarifa za utekelezaji kwa Mkuu wa wilaya na Mkuu wa Mkoa ambao ni sehemu ya Serikali Kuu, rejea kifungu cha 9(b) cha marekebisho ya sheria mbalimbali za Serikali za mitaa kinachorekebisha kifungu cha 174 cha sheria Mama ya Local Government District Authorities Act.
Kambi Rasmi ya Upinzani inaona huu ni udhibiti badala ya ushauri ili kudhibiti taarifa za Serikali za mitaa zinazotakiwa kupelekwa Serikali Kuu.

**44. Mheshimiwa Spika,** Ni ukweli kwamba marekebisho hayo yaliyofanyika badala ya kutoa madaraka zaidi kwa Serikali za Mitaa ndiyo yanazidisha kupokwa madaraka kwa Serikali za Mitaa. Hii ni hatari sana na inaonyesha kwamba marekebisho hayo yalikuwa na agenda ya siri kwani ilionekana wazi kwamba Vyama

shindani na Chama Tawala vinaweza kushinda uchaguzi katika ngazi za halmashauri na kuendesha Halmashauri. Hivyo marekebisho hayo yalifanyika kwa nia ovu ya kuendelea kudhibiti halmashauri na kutawala kwa mlango wa nyuma.

Ni muda mwafaka sasa kurekebisha mfumo wetu wa utawala wa Serikali kuu kutoka kwenye udhibiti na kuwa usaidizi na uangalizi zaidi

**45. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri serikali kwamba kama nchi hii inataka Kufikia maendeleo ya haraka ni lazima iondoe huu muingiliano wa maagizo na maekekezo kwenye halimashauri za nchi hii ambapo kwa upande mmoja kuna Madiwani na upande wa pili kuna wakuu wa mikoa ,wilaya na Waziri mwenye dhamana na hata viongozi wa chama tawala wote wakitoa maagizo na Maelekezo kwa Mkurugenzi na manejimenti yake ya halimashauri jambo linalowakwaza sana wakurugenzi na watumishi wengine kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## X. KODI YA MAJENGO (PROPERT TAX)

**46. Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa halmashauri hapa nchini zimekuwa zikikusanya mapato kwa ajili ya kuendesha miradi yake ya maendeleo na shughuli nyingine za kawaida kutoka kwenye vyanzo vyake vya

mapato kwa mujibu wa sheria ya fedha ya Halmashauri (Local Government finance Act, 1982) haukuwa uamuzi sahihi kutunga sheria ya kuondoa chanzo cha mapato cha kodi ya majengo kutoka katika halimashauri nchini .

**47. Mheshimiwa Spika**, Kufutwa kwa kifungu kilichokuwa kinazipa Halmashauri jukumu la kukadiria na kukusanya kodi za majengo na kulihamishia TRA kupitia sheria ya fedha ya mwaka 2016, kifungu cha 38 baada ya kufanya marekebisho kwa kuvifuta vifungu vya 31A na 31B vya sheria ya fedha ya Serikali ya Mitaa sura 290 kumeziyumbisha sana halimashauri katika kutekeleza majukumu yake kutokana na ukweli kwamba chanzo cha kodi ya majengo kilikuwa ni mojawapo ya chanzo kikubwa cha mapato hususani katika Manispaa na majiji hapa nchini.

**48. Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali inaonyesha kodi ya Majengo iliyokusanywa ni shilingi milioni 4,762.37 kati ya mIlioni 29,004 sawa na asilImia 17.4 tu.

Sababu ya makusanyo hayo madogo imeelezwa kuwa ni pamoja na kutokamilisha maandalizi ya yatakayowezesha ukusanyaji ikiwa ni pamoja na kuandaa sheria na kanuni za ukusanyaji ,kutengeneza Mfumo wa ukusanyaji wa kodi ,kuunda kitengo ,kuweka wafanyakazi na vitendea kazi.

**49. Mheshimiwa Spika**, Halmashauri zote kwa muda wa miaka zaidi ya 30 ya uhai wa serikali za mitaa zimeimarisha miundombinu ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato na rasilimali watu ambapo ilikuwa inahitaji marekebisho ya kawaida kuongeza ufanisi hususani kuziruhusu halimashauri ziajiri watumishi zaidi kwenye idara za fedha za halimashauri.

Maoni ya wabunge wengi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye hotuba ya bajeti mwaka 2016/17 yalikuwa ni kutoondoa chanzo hIcho cha kodi ya majengo katika halmashauri lakini serikali ikakataa ushauri huo kwa msisitizo kwamba TRA ina uwezo Wa kukusanya.

Serikali illiahidi kwamba baada ya kukusanya itarejesha Fedha hizo kwenye halmashauri jambo ambalo halijafanyika mpaka sasa kwa halmashauri nyingi nchini.

**50. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kama kweli tunahitaji kuendelea na Sera ya D by D ambayo ina lengo la kutoa mamlaka kamili kwa Serikali za mitaa ni lazima serikali ipitie upya sheria ya Property tax ili jukumu la makusanyo ya kodi hiyo liendelee kufanywa na halimashauri kwavile ukweli uko wazi kwamba TRA wanajukumu kubwa sana la kupanua wigo wa walipa kodi na jukumu kubwa la kuvisimamia vyanzo vyake ambavyo bado havijakusanywa kwa ufanisi.

## XI. ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI KATIKA MIJI YA TANZANIA

**51. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na uchukuzi-Sekta ya mawasilIano imefanya kazi kubwa ya Kuandaa Mfumo wa Anwani za makazi na Postikodi na kufanyia majariblo baadhi ya maeneo katika halimashauri hapa nchini,

Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwenye sekta ya mawasiliano ambayo ndio inaratibu program hii na pIa kuzielekeza halimashauri kutenga fedha kwenye bajeti zake ili mradii huu wa Anwani za makazi na Postikodi ukamilike kwa haraka kwa lengo la kurahisisha mawasiliano na ukusanyaji wa mapato kwa Serikali kuu na seriSerikali za mitaa.

## XII. WATUMISHI HEWA TAMISEMI

**52. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwepo na zaoezi linaloendeshwa na Serikali kuu la kubaini watumishi ambao wanapokea fedha bila ya kufanya kazi kwa maana rahisi na iliyozoeleka wanaitwa watumishi hewa. Zoezi hili la kuhakiki watumishi hewa limepelekea kusitishwa kwa ajira mpya.

**53. Mheshimiwa Spika**, Ni ukweli kwamba vyeo vya RAS, DAS na DED sio nafasi za kisiasa na mtumishi

kufikia nafasi hizo ni dhahiri kwamba amepitia ngazi mbalimbali katika utumishi wa Umma. Ngazi hizo huendana na marupurupu na mshahara, na ni ukweli pia mtumishi katika nafasi hiyo akiondolewa kwa mujibu wa sheria haina maana kwamba na mshahara wake unaondolewa.

Nia ya serikali ya awamu ya tano ni kubana matumizi hivyo Ungetegemea mabadiliko yaliyofanywa ya Makatibu Tawala wa mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halimashauri ambao wote ni viongozi wa kitaaluma yazingatie nia hiyo ya kubana matumizi badala ya kutengeneza watumishi hewa ambao wanalitia taifa hasara kubwa.

Kwa mfano kati ya Wakurugenzi 184 wa Halimashauri hapa nchini,wakurugenzi 120 wa zamani hawakuteuliwa kwa nafasi hizo katika serikali ya awamu ya tano ambapo hata wale wapya walioteuliwa walitoka nje ya mfumo wa Utumishi wa Umma wengi wao wakiwa ni makada wa CCM. Baada ya kutenguliwa kwa wakurugenzi hao 120 kutoka halimashauri mbali mbali nchini walielekezwa kuhudhuria kwa Makatibu Tawala wa Mikoa waliyotoka kwa ajili ya kupangiwa kazi.

Ni zaidi ya Mwaka mmoja sasa Wakurugenzi hawa takribani wote wanahudhuria kwa Makatibu Tawala wa Mikoa ambapo kimsingi hawana kazi za kufanya

kwa kuwa ikama ya watumishi haionyeshi nafasi zao katika ngazi ya Katibu Tawala wa Mkoa.

Ikumbukwe kwamba Wakurugenzi hawa bado wanalipwa Mishahara yao pamoja na stahiki zingine za kiutumishi kama Nyumba, Umeme, simu, matibabu, n.k. Wastani wa mshahara wa Mkurugenzi ni Tsh. 3,820,000 mpaka Tsh.4,000,000kwa mwezi hivyo Malipo kwa wakurugenzi 120 ni takribani Tsh. 480,000,000 kwa mwezi na hivyo kwa mwaka ni takribani Tsh. 5,760,000,000.

Tafsiri sahihi ya jambo hili linaloendea ni kuwepo kwa Double' Payment' ya Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tawala wa zamani waliokuwa wameshafikia ngazi hizo za madaraka na Wale wapya ambao ndio walioteuliwa.

Aidha Serikali inaweza ikawa imejiingiza katika Ubadhirifu kwa matumizi ya zaidi ya Shilingi bilioni 5.76 kinyume cha fedha iliyopitishwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kutokana na ikama ya Wakurugenzi wa hapa nchini.

**54. Mheshimiwa Spika**,Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu sahihi juu ya sintofahamu hiyo ya waliokuwa Wakurugenzi wa Halimashauri,Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya ambao bado wanapokea Mishahara na stahiki zingine za madaraka kwa nafasi ambazo walishaondolewa.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na maumivu ya kisaikolojia (psychological toucher) waliyopata wakurugenzi wa zamani kutokana na Chuki,Ubaguzi na matumizi mabaya ya madaraka ya Mamlaka za uteuzi yaliyosababishwa na Matokeo ya Uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ambapo maeneo ambayo upinzani ulishinda Wakurugenzi wake hawakupata uteuzi kwa nafasi hizo kwa serikali hii ya awamu ya tano kwa kisingizio kwamba hawajakisaidia chama cha mapinduzi kupora ushindi halali Wa wapinzani.

**55. Mheshimiwa Spika**,Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali ya awamu ya tano ijiisahihishe ili ilsije ikiwafanya wananchi waamini kwamba Serikali ya Chama cha mapinduzi inahalisha vitendo vya wasimamizi wa Uchaguzi kuharibu uchaguzi Kwa kutangaza matokeo batili bila kuelewa kwamba vitendo hivyo vinahatarisha amani na utulivu wa nchi ya Tanzania. Na kwa maana hiyo kwa Serikali ya CCM ni heshima kwa msimamizi wa Uchaguzi kutotenda haki aliyoapa kuisimamia kwa mujibu wa Katiba ya nchi kwa kutumia vitabu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu huku akilipwa fedha za Walipa kodi wa Tanzania.

## XIII. TAARIFA YA LAAC

**56. Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ya mitaa kama

ilivyofanyia uchambuzi Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/14 na mwaka 2014/15 imeonesha maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za serikali za mitaa kama ifuatavyo:

a) Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011,
b) Kutotekeleza Mapendekezo ya Kamati kwa kipindi cha nyuma na kutojibu Hoja za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati, na
c) Usimamizi mbovu wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unaopelekea kuwepo kwa Miradi ya Maendeleo isiyo kamilika kwa muda mrefu, miradi inayokamilika lakini haitumiki kama ilivyokusudiwa, na baadhi ya miradi kukamilika ikiwa katika ubora wa hali ya chini kinyume na matakwa ya mkataba.

**57. Mheshimiwa Spika**, Maeneo mengine yenye matatizo sugu ni pamoja na:

a) Baadhi ya Halmashauri kutochangia kabisa na nyingine kutochangia kikamilifu na kwa wakati, asilimia kumi (10%) ya fedha kutoka katika mapato ya vyanzo vya ndani (own sources revenue) kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana,
b) Baadhi ya Halmashauri kutokupeleka kabisa na nyingine kutopeleka kikamilifu asilimia ishirini (20%)

ya ruzuku inayopokelewa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya Mamlaka za Chini (Vijiji na Serikali za Mitaa);

c) Uzembe katika ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri na upotevu usio na maelezo ya kuridhisha wa Vitabu vya Wazi vya kukusanyia mapato;
d) Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuchelewa kutolewa na Hazina au kutototolewa kabisa;
e) Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani (weak internal control system);
f) Watumishi kukaimu Nafasi zao bila kuthibitishwa kwa muda mrefu; na
g) Kubadili matumizi ya fedha kinyume na bajeti kwa kutumia kivuli cha maagizo kutoka ngazi za juu.

**58. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri serikali kwamba panahitajika jitihada za ziada katika kuboresha matumizi ya fedha za umma na kuzingatia sheria ya fedha na manunuzi.

## XIV. HATI ZINAZOTOLEWA BAADA YA KUFANYIKA KWA UKAGUZI WA MAHESABU

**59. Mheshimiwa Spika**, Hati zinazotolewa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali mara nyingi ni kuonesha ni jinsi gani fedha zilivyotumika. Hati

zinazoridhisha, Hati zenye shaka, Hati zisizoridhisha na Hati Mbaya.

**60. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba mbali ya juhudi nyingi zinazofanywa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na matumizi makubwa na mabaya ukweli ni kwamba mara nyingi ukaguzi huo unafanyika wakati tayari fedha zimekwishatumika.

**61. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani ina imani kwamba kitengo cha ukaguzi wa ndani kikiimarishwa ni dhahiri ndicho kitakachosaidia kuzuia wizi badala ya kutafuta jinsi fedha zilivyoibwa.

Aidha itakuwa vizuri sana kama wakaguzi wa ndani watakuwa wanahamishwa vituo vyao vya kazi mara kwa mara badala ya kuwa katika kituo kimoja kwa muda mrefu kwani jambo hilo linatengeza mahusiano ya karibu sana na Maafisa masuhuli na wasaidizi wao jambo ambalo linahatarisha umakini katika usimamizi wa raslimali za halimashauri.

## XV. UTEKELEZAJI WA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI

**62. Mheshimiwa Spika**, Tamisemi ndio wasimamizi wakuu wa elimu ya msingi na elimu ya sekondari hapa nchini, lakini watoa miongozo ya jinsi ya kuendesha elimu hiyo ni serikali kuu. Kwa maana hiyo mamlaka inayotoa leseni na vibali vya uanzishwaji wa shule ni Serikali kuu.

**63. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba matatizo wanayokumbana nayo Tamisemi kuhusu uendeshaji wa elimu katika ngazi hiyo chimbuko lake ni Serikali kuu. Tunasema hivyo kwa sababu, shule zinapewa vipi vibali vya kutoa elimu kwa wanafunzi bila ya kuwa na vyoo, madarasa na madawati, viwanja vya michezo n.k? Kwa kuwa shule hizo zinamilikiwa na Halmashauri zetu hivyo ni jukumu la msingi la halmashauri hizo kuweka miundombinu tajwa hapo juu ili kukidhi matakwa ya usajili wa shule hizo. Hivi ni kwa nini shule binafsi hazina tatizo la vyoo, madarasa, madawati na viwanja vya michezo?

**64. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya awamu ya tano imeazimia kutoa/ kutekeleza dhana ya elimu bure kwa elimu ya msingi na sekondari, pamoja na dhana hiyo hakuna ufafanuzi wa kutosha au unaoeleweka. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali:-

**Kwanza,** kuweka wazi kwa umma wa Tanzania vipengele vyote ambavyo havitachangiwa na wananchi ili kuondoa mkanganyiko uliopo na kuwezsesha bajeti za ukweli kuandaliwa.

**Pili**, ili kuwezesha upatikanaji wa elimu bora vijijini na mijini katika ngazi ya msingi na sekondari, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupeleka bajeti kamili kwa ajili ya kujenga shule zilizokamilika, yaani pasiwe na shule inayojengwa bila kukamilisha darasa, sambamba na

uwiano wa madawati na vyoo vinavyoendana na idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa.

**Tatu,** Kwa kuwa Serikali imeweka vigezo/viwango **(standards)** stahili kwa ajili ya kusajili shule za msingi na serikali basi bajeti inayopelekwa katika halmashauri ni lazima itosheleze kujenga miundombinu ya shule za umma katika viwango vilivyowekwa na serikali yenyewe.

**65. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba, katika enzi hizi za maendeleo ya viwanda kuelekea Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa Kati haitawezekana watoto wetu katika shule za msingi na sekondari waende katika shule zisizokidhi viwango hususani ukosefu wa matundu ya vyoo na madawati.

**66. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba, ni muda mwafaka sasa kwa Serikali kuangalia chombo ambacho kitasimamia kwa haki mfumo wa utoaji wa elimu hapa nchini.

## ELIMU YA MSINGI

**67. Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Elimu na ile ya TAMISEMI kupitia (LGDG) inajumuisha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa programu za Elimu ya Elimu ya Msingi na Sekondari katika ngazi za Halmashauri. Taarifa ya utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Utawala na S/Mitaa kwa kipindi cha

2016/17 inaonesha kuwa kuna ongezeko kubwa la uandikishaji wa wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari katika mwaka huo wa fedha ikiwa ni ongezeko la takriban wanafunzi 509,085 wa Msingi na katika shule za sekondari ongezeko la wanafunzi 64,562 nchi nzima.

**68. Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Elimu Bure ulianza Jan 2016, hivyo kati ya Jan-June 2016, Serikali ilijipanga kushughulikia upungufu uliokuwepo kwa kuhakikisha kwamba Halmashauri na wadau wengine wa sekta ya Elimu wanachangia kwa hali na mali kupunguza makali ya upungufu huo. Taarifa inaonesha wazi kuwa kwa ujumla wake, Serikali na wadau wamefanikisha kuwepo kwa "ziada ya Madawati 66,042 (msingi) na 45,015 sekondari katika baadhi ya Halmashauri na Mikoa" Lakini wakati huo huo taarifa hiyo bila kutaja mikoa yenye ziada, inaonesha upungufu wa madawati 28,922 (msingi) na 3,875 (sekondari), na kuelezea bayana kwamba upungufu huo unaendelea kufanyiwa kazi.

**69. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuna kukosekana kwa umakini katika mifumo ya uratibu na ufuatiliaji kuliko sababisha kuwa na ongezeko kubwa la madawati "katika baadhi ya halmashauri na mikoa" kitu ambacho kimesababisha usumbufu mkubwa na matumizi yasiyokuwa na lazima ya fedha kutengeneza madawati ambayo hayakuhitajika na kwa sasa hayatumiki.

**70. Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, ni utaratibu uliotumiwa na Ofisi ya Bunge kutengeneza madawati kwa kulitumia jeshi la Magereza na kuwagawia waheshimiwa wabunge, haukuwa mzuri na umezitia hasara kubwa halmashauri zetu. Mfano, Halmashauri za Tarime, Ukerewe, Moshi Vijijini, Bukoba Mjini na zinginezo za Ukanda wa Ziwa kutakiwa kufuata madawati mkoa wa Ruvuma na Lindi kwa gharama ambazo zingeweza kutengeneza mara mbili madawati hayo kwenye maeneo yao, Jambo hili liliongeza matumizi yasiyokuwa kwenye bajeti za Halmashauri nyingi hapa nchini.

**71. Mheshimiwa Spika,** Utengenezaji wa madawati kwa kutumia takwimu za ujumla za ongezeko la uandikishaji linaweza kupotosha bajeti za mpito na hata bajeti kuu, kwani uhalisia haupo kama inavyofikiriwa kinadharia. Inasikitisha kuona katika Halmashauri na mikoa mingine madawati yaliyogharimu fedha nyingi yakipigwa jua au yakinyeshewa mvua kwa kukosa mahali pa kuyahifadhi.

## XVI. KUIMARISHA MICHEZO NA UTAMADUNI KATIKA HALMASHAURI

**72. Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Michezo na utamaduni katika halimashauri zinakuwa chini ya idara ya Elimu ya Msingi ambayo ina majukumu makubwa sana ya kushughulikia elimu ya Msingi na sehemu kubwa ya bajeti yake ya matumizi ya kawaida inatoka serikali kuu.

Kitengo cha Michezo na utamaduni kinakuwa kimemezwa na shughuli za Elimu ya Msingi hivyo kushindwa kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.

**73. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri serikali kuunda idara mpya ya Michezo na utamaduni katika halimashauri hapa nchini ili kuinua na kuhamasisha shughuli za Michezo na utamaduni katika nchi yetu kwavile zitalazimisha serikali kuu na Halimashauri kutenga fedha za kutosha katika bajeti kwa ajili ya idara hiyo ya Michezo na utamaduni.

## XVII. UTOAJI WA HUDUMA YA AFYA

**74. Mheshimiwa Spika**, Dira ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 ni kuwa na jamii yenye afya ambayo itachangia kikamilifu kati ka maendeleo binafsi na ya taifa kwa ujumla. Pia sera hiyo inakusudia kutoa huduma muhimu za afya zenye uwiano wa kijiografia, viwango vya ubora unaokubalika, gharama nafuu na zilizo endelevu.

**75. Mheshimiwa Spika,** Tanzania inakadiriwa kuwa na takriban zahanati zipatazo 4679, vituo vya afya 481 pamoja na hospitali 219. Zahanati na vituo vya afya ndizo nguzo kuu za huduma za afya ya msingi kwani hutoa huduma za awali kwa watanzania kati ya elfu kumi (10,000) kwa Zahanati na elfu hamsini (50,000) kwa kituo cha afya. Hata hivyo kasi ya ongezeko la idadi ya watu, upungufu wa

watumishi wenye sifa, upungufu wa nyenzo, madawa, umbali wa vituo vya kutolea huduma, ubovu wa barabara za vijijini pamoja na tatizo la usafiri wenye uhakika ni changamoto kubwa zinazokabili utoaji wa huduma za afya ya msingi hapa nchini.

**76. Mheshimiwa Spika,** katika utoaji wa huduma za afya, sekta binafsi inamchango mkubwa, Kwa sasa asilimia arobaini (40%) ya vituo vyote vya huduma za afya nchini, vinamilikiwa na watu binafsi. Changamoto kubwa kwa sasa ni kuwa zaidi ya asilimia 90% ya vituo binafsi vipo mijini na kuacha asilimia kubwa ya watanzania takribani 80% inayoishi vijijini kukosa huduma muhimu za afya.

## XVIII. MFUKO WA BIMA YA AFYA YA JAMII-CHF

**77. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuboresha mfumo wa Bima ya Afya ya jamii –CHF ili kuwezesha wanachama wa mfuko huu waweze kinufaika kwa kupata huduma mahali popote hata nje ya eneo analoishi. Mfano; Mwanachama aliyeko Kibakwe au Kongwa, aweze kupata huduma hata akiwa Peramiho au Ukerewe n.k Pia suala la huduma ya afya kwa wazee litiliwe mkazo na Halmashauri zote ziwekewe muda maalum kuhakikisha kuwa wazee wote wanapata vitambulisho na kupata huduma za afya.

## XIX. MASLAHI YA WATUMISHI KATIKA SEKTA YA AFYA NA ELIMU

**78. Mheshimiwa Spika**, kushuka kwa ari ya kazi kwa watumishi katika halmashauri zetu inachangiwa na mambo kadhaa na hivyo kupunguza kasi ya ubunifu na bidii katika kutoa huduma kwa wananchi, baadhi ya mambo hayo ni:

a. Kutopandishwa madaraja kwa watumishi mbalimbali hasa walimu na watumishi wa afya
b. Kutokupata nyongeza ya mishahara kwa wakati,
c. Kukaimishwa kwenye nafasi mbalimbali kwa muda mrefu bila kuthibitishwa licha ya kuwa na sifa stahiki.

**79. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha mapungufu haya na mengine ambayo hatukuyataja yanafanyiwa kazi kwa haraka ili kwenda sambamba na Dira ya Sera ya Afya ya mwaka 2007.

## XX. UMASKINI NA VIASHIRIA VYA UMASIKINI

**80. Mheshimiwa Spika,** Umaskini ni hali ya maisha isiyoridhisha. Ni hali ya kuwa na uwezo mdogo wa kumudu mahitaji ya maisha ya mwanadamu ya kila siku. Hali hii inajidhihirisha; kwa kuwa na kipato duni, kuishi katika mazingira duni, kusumbuliwa na maradhi na ujinga.

Kambi Rasmi ya Upinzani imelazimika kuweka hiyo tafsiri ya umasikini kwa sababu kubwa kwamba, utendaji wa Serikali za Mitaa ndio chombo au mamlaka pekee ya kisheria

inayoweza kuiondoa jamii ya kitanzania katika umasikini nasio serikali kuu.

**81. Mheshimiwa Spika,** Nchi yetu kinadharia ina muundo **(Structure)** mzuri sana wa Serikali za Mitaa ambapo mfumo wake unaanzia ngazi za kamati za mitaa, mikutano ya mltaa, mikutano ya vitongoji ,Halmashauri za vijiji na mikutano ya vijiji.

Kuna ngazi ya Kamati ya maendeleo ya Kata na hatimaye ngazi ya halmashauri kabla ya ngazi ya Serikali Kuu ambayo ni pamoja na Tarafa, Wilaya, Mkoa na Wizara yenye dhamana na Serikali za Mitaa.

**82. Mheshimiwa Spika,** Mfumo huu ukiratibiwa vizuri kwa maana ya kuruhusu kwa vitendo maamuzi kutoka chini kwenda juu (Bottom-Up) maendeleo ya nchi hii yatapatikana kwa haraka sana.
Ni ukweli kwamba maendeleo hayo yatagusa watu katika nyanja za kIuchumi,kisiasa na kijamii. Hivyo Taifa litaweza kuvipunguza sana viashiria vya umasikini.

## XXI. VIASHIRIA VYA UMASKINI

**83. Mheshimiwa Spika,** Viashiria vinavyoonyesha hali halisi ya umaskini hapa Tanzania ni pamoja na:

i. kutojua kusoma na kuandika,

ii. Kutokuwa na uhakika wa kupata chakula, mavazi na malazi.
iii. Uhaba wa maji safi na salama,
iv. Huduma duni za afya,
v. Vifo vingi vya wananchi,
vi. Muda mfupi wa maisha,
vii. Utapiamlo kwa watoto na watu wazima,
viii. Uchakavu wa mazingira,
ix. Ukosefu wa ajira na kipato duni,
x. Kutofahamu masuala muhimu ya jamii.

**84. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini na kuendelea kusisitiza kwamba Serikali za Mitaa ndio mamlaka sahihi yenye uwezo wa kupamba na umasikini kutokana na mfumo wake wa kiutendaji, vilevile ndio mamlaka inayoweza kutoa takwimu sahihi kwa ajili ya kupanga jinsi ya kugawa raslimali (planning and allocation of resources) katika suala zima la kupambana na umasikini. Hivyo ni vyema Serikali ya awamu ya Tano ikatengeneza mkakati thabiti wa kuimarisha Serikali za Mitaa kama mpango ulivyobainishwa katika Programu ya maboresho ya Serikali za mitaa.

## XXII. UMUHIMU WA KUTUMIA MAWAKALA KATIKA KUKUSANYA MAPATO

**85. Mheshimiwa Spika**, Serikali za Mitaa zinakusanya mapato kupitia ada, ushuru, faini na kodi mbalimbali

kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Mamlaka husika kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Namba 9 ya mwaka 1982,

Baadhi ya masuala yanayozungumziwa katika sheria hii ni pamoja na vyanzo vya mapato, taratibu za kutoza kodi na ukusanyaji wa mapato, matumizi ya fedha, usimamizi wa fedha pamoja na ukaguzi wa vitabu. Kwa ujumla, sheria hii inakazia juu ya usimamizi na udhibiti wa mali za Halmashauri ambazo zinahusisha fedha taslimu na rasilimali nyingine.

**86. Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa kukusanya kodi na ushuru ni kwa mujibu wa sheria ya fedha kama ilivyonukuliwa hapo awali, vivo hivyo na utoaji wa huduma za msingi kwa wananchi pia ni jukumu la halmashauri.

**87. Mheshimiwa Spika,** Utaratibu wa kukusanya mapato katika halimashauri kwa kutumia mawakala ulifanyiwa utafiti kwa Msaada wa benki ya Dunia kwa miaka kadhaa ambapo ulienda sambamba na sera ya maboresho ya serikali za mitaa.

Utaratibu huu kwa baadhi ya halimashauri za Manispaa na majiji hapa nchini umeshatumika kwa zaidi ya miaka kumi.

Mwaka hadi mwaka kumekuwa na mafanikio makubwa katika kuongeza mapato ya halimashauri kwa kutumia utararatibu huo, hivyo usingetegemea Serikali makini ikurupuke kutaka kufuta utaratibu huo kutokana na changamoto ambazo ni rahisi kukabiliana nazo.

**88. Mheshimiwa Spika,** Utaratibu wa awali wa kuwapa mawakala viwango vya kuleta katika halmashauri ulikuwa na faida kwa halimashauri na serikali kwasababu zifuatazo:

i. Gharama zake zake za ukusanyaji zilikuwa zenye tija (cost effective)
ii. Halmashauri zilikuwa zinapata fedha za dhamana kabla ya wakala kuanza kazi hivyo hata kama wakala akishindwa katikati Halmashauri ilikuwa haipati hasara.
iii. Utaratibu wa kulipa commission kwa mawakala unakuwa hauna uhakika kwa mzabuni kumaliza mkataba wake.Vilevile kunakuwa na visingizio vingi vya wazabuni kutoa taarifa ya hasara na hivyo ama kutishia kujitoa au kujitoa kabisa jambo ambalo linaziweka halimashauri katika wakati mgumu sana wa mapato.
iv. Ushindani wa wazabuni katika tenda ulikuwa mkubwa kiasi kwamba halimashauri makini zilikuwa zinaongeza mapato mwaka hadi mwaka.
v. Halimashauri zilikuwa zinapata msingi wa kutengeneza 'data base' za mapato kupitia katika ushindani wa wazabuni katika tenda.
vi. Utaraibu wa mwanzo umesaidia sana kutengeneza ajira kwa kuimarisha sekta binafsi hivyo kuzipunguzia halimashauri mzigo wa kuajiri vibarua wengi ambao

wangefanya matumizi ya mishahara yawe makubwa sana katika halimashauri zetu.

**89. Mheshimiwa Spika,** Kuna vyanzo katika halimashauri havikusanyiki kabisa katika Mfumo huu wa kutumia 'commission' kwa asilimia isiyozidi ishirini jambo ambalo limeathiri ukusanyaji wa mapato kulingana na bajeti za halimashauri.

**90. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaIshauri Serikali kwamba kutokana na uzoefu ilioupata kutoka kwenye halimashauri zilizo chini yake ni muhimu Ofisi ya Rais TAMISEMI ifanyie mapitio maagizo na miongozo yake kuhusiana na utaratibu mpya wa kutumia mawakala katika kukusanya mapato.

Pia ni vizuri Ofisi ya Rais TAMISEMI ikazipitia changamoto zote zilizopatikana kwa kipindi cha mwaka mmoja katika utaratibu mpya wa kutumia mawakala kwa kuwalipa 'commission' isiyozidi asilimia ishirini kutokana na mapato yaliyokusanywa katika Halimashauri ili waone haja ya kurudi kwenye utaratibu wa zamani wa kuwapa mawakala kiwango cha kulipa katika halimashauri baada ya kushindanishwa katika taratibu za zabuni bila kujali kwamba wakala ametumia kiasi gani cha gharama katika ukusanyaji.

## XXIII. FEDHA ZA OC NA FEDHA ZA MAENDELEO KUTOFIKA KWA WAKATI

**91. Mheshimiwa Spika,** General purpose grant (Ruzuku ya serikali kuu kwa vyanzo vilivyofutwa) ni muhimu iletwe kwenye halimashauri kwa wakati ili asilimia ishirini iweze kuelekezwa kwenye vijiji na mitaa. Pia fedha za Ruzuku kwa miradi ya Maendeleo laziima zifike kwa wakati. Hii ruzuku sio hisani bali ni kwa mujibu wa sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa kifungu cha 10, kuchelewa kutolewa kwa fedha hizo maana yake ni kuchelewesha maendeleo kwenye maeneo husika. Hivyo basi ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuitaka Serikali kuhakikisha ruzuku husika inapelekekwa kwa wakati ili iwe na maana zaidi kiutendaji, kwani kuchelewesha fedha hizo kunazidisha uwezekano wa ubadhirifu wa fedha hizo pindi zinapotolewa kwa kuchelewa.

**92. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali Kujenga imani kwa wananchi kwa kuhakikisha bajeti ya miradi ya Maendeleo inatekelezwa kwa wakati katika halimashauri hapa nchini ili kuwafanya wananchi wawe na moyo katika kushiriki vikao vya kuibua miradi katika ngazi za nchini.

## XXIV. AKAUNTI MAALUMU KWA FEDHA ZA MFUKO VIJANA NA KINAMAMA

**93. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha kuwa Halmashauri inatenga asilimia kumi (10%) ya mapato yake yote kwa ajili ya mfuko wa maendeleo wa wanawake (5%) na wa vijana (5%) na kuhakikisha fedha hizo zinakopeshwa kwa

walengwa baada ya kujiridhisha kuwa walengwa wana sifa za kukopeshwa kwa sababu mfuko huo ni endelevu (revolving fund).

**94. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa kila Halmashauri ifungue akaunti maalum ili fedha hizo ziwekwe huko ili zisiwekwe kwenye General akaunti ambapo wakati mwingine fedha hizo zinaweza kutumika kama matumizi mengineyo (OC) na hivyo kushindwa kubainika matumizi yake. Kwa kuwa na Akaunti Maalum kutasaidia marejesho ya fedha hizo kutoka kwa wanufaikaji kurejeshwa kwenye akaunti hiyo na itakuwa rahisi kuiratibu au kuifanyia ukaguzi.
Kwa hali illvyo sasa ni vigumu kutenganishwa fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka na zile ambazo ni marejesho ya wakopajI.

## XXV. POSHO KWA VIONGOZI WA KUCHAGULIWA

**95. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa ni kilio cha muda mrefu kwa viongozi wa kuchaguliwa kutaka ama kuongezewa posho au wengine kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa kupata posho.
Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali ijitahidi kuboresha posho za madiwani kufikia kiasi kisichopungua laki nane( Tshs 800,000)kwa mwezi ikiwa ni pamoja na posho za vikao kufikishwa elfu sabini(Tshs 70,000), Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali izielekeze Halimashauri

kutenga fedha katika bajeti zao ili ziweze kuwalipa wenyeviti wa vijiji mitaa na vitongoji posho isiyopungua elfu hamsini(Tshs 50,000) kwa mwezi na elfu ishirini(Tshs 20,000)kwa wajumbe wa halimashauri za vijiji na wajumbe wa kamati za mitaa.

**96. Mheshimiwa Spika,** Tunatoa pendekezo hilo kutokana na ukweli kwamba, ngazi hii ya kiutendaji ndiyo muhimu sana katika maendeleo ya nchi kwani ndiko maendeleo yanakotakiwa kutekelezwa na ndipo umasikini ulipo. Hivyo kiasi hicho cha fedha ni kutoa motisha kwa viongozi wetu ili waongeze bidii Katika kutekeleza majukumu yao. Tukumbuke kwamba watendaji wa vijiji na mitaa hawawezi kufanya kazi zao bila kuwategemea viongozi hao waliochaguliwa na wananchi. Watendaji (VEO na WEO) ni waajiriwa wa Serikali lakini wenyeviti na wajumbe wanafanyakazi katika mazingira magumu na hivyo kupelekea uwezekano wa kuwepo na rushwa ndogo ndogo ambazo zinazidisha kero kwa wananchi badala ya kutatua kero za wananchi

## XXVI. USAFI WA MAZINGIRA

**97. Mheshimiwa Spika,** Hoja ya usafi wa mazingira kwa miji yetu limekuwa ni jambo ambalo kwa kiasi kikubwa likitia doa halmashauri zetu, kutokana na ukweli kwamba Halmashauri nyingi zimeshindwa kuwa na utaratibu unaoleweka wa kushughulika na taka ngumu.

**98. Mheshimiwa Spika,** Tunaposema uwezo maana yake ni Halmashauri kutokuwa au kuwa na fedha kidogo kwa ajili ya kuthibiti taka hizo.
Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali izielezekeze halimashauri kutenga bajeti kwa ajili ya kuendesha program ya kudhibiti taka ngumu (sold waste management) ikiwa ni pamoja ni kuelimisha wananchi namna ya kutenga taka taka katika vyanzo vya kukusanyia taka hizo (separation at source). Programu hii itahusisha mpango wa kutenganisha taka kulingana na matumizi kwa aina ya taka (Renewal, Reuse and Recycling -3Rs). Lengo kubwa la programu hii ni kubadilisha mitazamo ya wananchi wanaoamini kwamba taka taka ni uchafu badala yake kuwa rasilimali.

**99. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba kama mpango huu ukitekelezwa vizuri utasaidia miji yetu kuwa safi kwa gharama nafuu zaidi na pili halimashauri zetu kuwekeza kwenye 'Recycling plants' 'Composite manure plants','Methane gas na Bio gas plants' ambacho kitakuwa chanzo cha mapato na pia kuwa na uhakika wa kutoa ajira kwa vijana wetu.

**100. Mheshimiwa Spika,** Aidha Kamati za mazingira za Halmashauri zikiwemo za kwenye kata ni muhimu ziimarishwe ili jukumu la kukabiliana na uchafuzi wa mazingira litekelezwe vizuri kwenye ngazi za chini ambapo ndipo wananchi wapo.

## XXVII. BUGHUDHA NA MAPAMBANO DHIDI YA WAFANYABIASHARA WADOGO (WAMACHINGA) KATIKA MIJI, MANISPAA NA MAJIJI

**101. Mheshimiwa Spika,** Swala la Wamachinga katika nchi ya Tanzania linatakiwa lipate mtazamo mpya kutoka kwa viongozi wa serikali. Kutokana na kukosekana kwa ajira rasmi watu wengi wanawake na wanaume wameamua kujiajiri wenyewe kwenye biashara ndogo ndogo ili kukidhi mahitaji yao ikiwemo chakula, Malazi, mavazi, Elimu, matibabu n.k

Utashi huo wa wananchi kujishughulisha na biashara ndogo ndogo kwanza unaongeza pato la Taifa na pili unasaidia sana kundi kubwa haswa la vijana kutojihusisha na vitendo vya uhalifu kama wizi, ujambazi, uzuzuraji n.k

Vitendo vya uhalifu vinapopungua inakuwa ni faraja kwa kundi la matajiri,watu wa kipato cha kati ,na hata viongozi wetu. Pia inasaidia utulivu wa nchi hivyo vyombo vya ulinzi na usalama navyo vinakuwa na kazi ndogo ya kupambana na uhalifu.

**102. Mheshimiwa Spika,** Jambo muhimu sana ambalo viongozi mbali mbali wanapaswa kulifahamu ni kwamba kundi hili ndilo ambalo baadaye linazalisha watu wanaopata mafanikio makubwa kimitaji na hatimaye kuwa wawekezaji mashuhuri na muhimu katika uchumi wa nchi.

Mifano ipo mingi nje na ndani ya nchi ambapo Wajasiriamali wa sekta isiyo rasmi ndio baadhi yao walirasimishwa kutokana na kukuwa kwa Mitaji yao na leo ni matajiri wakubwa sana katika nchi zao wakiwa wanamiliki mitaji mikubwa sana.

**103. Mheshimiwa Spika,** Ni muhimu sana serikali ya Tanzania ikiwa ni pamoja na serikali za mitaa kubadili mitazamo yao juu ya Wamachinga ili iwatengenezee mazingira rafiki kwa biashara zao badala ya kuwa kikwazo kwao. Pia Viongozi mbali mbali wakiwemo Mawaziri, Makatibu wa Wizara Wakuu wa Mikoa,Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri lazima wabadili mitazamo yao ya kuwaona Wamachinga kama watu wanaovunja sheria za mipango miji hivyo kila wakati kutoa maagizo ya kuwakamata na kuwasumbua tena kwa kuwanyanganya Mali zao.

**104. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri serikali kutoa maagizo yenye msImamo wa pamoja,unaoeleweka na kuaminika kwa Wamachinga kuzielekeza halimashauri zote hapa nchi wakiwemo Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwamba zoezi lolote la kuwabughudhi Wamachinga kwa kutumia nguvu nyingi ni unyanyasaji usiozingatia haki na utu wa watu wanaojitafutia riziki yao halali haswa katika nchi ambayo kuna upungufu mkubwa wa ajira ulisababishwa kwa kiwango kikubwa na sera mbovu za ubinafisishaji za Serikali ya CCM .

## XXVIII. SHERIA NDOGO ZA HALIMASHAURI

**105. Mheshimiwa Spika,** Halmashauri lazima ziongezewe uwezo wa viwango vya faini kwa baadhi ya makosa. Kwa mfano uharibifu wa barabara kwa magari makubwa yanayoharibu barabara za lami katika halimashauri zetu lazima udhibitiwe kwa kutozwa faini inayozidi elfu hamsini.
Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri serikali kupitia upya sheria ndogo na adhabu zake ili izifanye ziende na wakati kutokana na mazingira halisi ya miji yetu bila kuleta bughudha kwa wananchi.

## XXIX. MATUMIZI MABAYA YA MADARAKA YA WAKURUGENZI WA HALIMSHAURI NA MANISPAA ZA MIJI

**106. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa waheshimiwa madiwani kwamba watumishi wa Halmashauri kusimamishwa kazi bila ya kufuata sheria na taratibu, jambo ambalo halmashauri inashtakiwa na kulazimika kuwalipa fidia, hivyo kuiingizia halmashauri hasara. Watendaji wa vijiji takriban 30 ambao ni watumishi wa umma kusimamishwa kazi kwa hisia za kisiasa, na hivyo kuathiri shughuli za maendeleo, hii imetokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru.

**107. Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na tabia ya wakurugenzi kutoa maelekezo ya kuwarudisha kazini

watumishi waliopatikana na makosa mbalimbali ya kinidhamu bila kuwapa adhabu yoyote pamoja na ushahidi wa wazi wa ubadhirifu. Na wanarudishwa kazini bila mchakato wa kinidhamu wa kisheria, hii ni kudharau mamlaka zilizowafanyia mchakato na hadi kuonekana kuwa makosa yametendeka. Mfano ni Mkurugenzi wa Hanang' na pia Meru.

**108. Mheshimiwa Spika,** Aidha, kumekuwa na utaratibu unaotumiwa na wakurugenzi wa kubadilisha matumizi ya fedha kama ambazo tayari zimepangiwa matumizi kwa bajeti zinazopitishwa na vikao vya baraza la madiwani bila ya kufuata utaratibu.Tukumbuke kwamba taratibu za operations zinazozuka toka juu zinakuwa hazina bajeti yoyote ya utekelezaji wake katika ngazi za chini.

**109. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema vitendo hivi vya wakurugenzi vinakwenda kinyume na sheria na miongozo ifuatayo:

1. Sheria ya madaraka Mikoani (The Regional Administration Act, sura 97 na marejeo ya 2002)
2. Sheria Na.7 Sura 287 ya mwaka 1982 (marejeo ya 2002)
3. Kifungu cha 43(5),(6) na (8) cha sheria ya fedha za mitaa Na.9 ya mwaka 1982 na marejeo yake ya 2002
4. Kifungu cha 5 na 6 cha mwongozo wa fedha za Serikali za mitaa(***local Government financial memorandum***) 2009

**110. Mheshimiwa Spika**, Utaratibu wa Tume ya Uchaguzi kuwatumia wakurugenzi wa halmashauri wakati wa Uchaguzi wa wakilishi wa wananchi wakati wakurugenzi hao wameteuliwa katika misingi yenye harufu za itikadi za kisiasa unakandamiza misingi ya Haki na Demokrasia katika nchi yetu.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuitengea tume ya Uchaguzi fedha za kutosha katika bajeti ili iajiri watumishi wa kutosha watakaoweza kusimamia haki wakati wa chaguzi mbali mbali hapa nchini.

## XXX. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2016/17 NA MPANGO WA MAENDELEO 2017/18 TAMISEMI (fungu 56)

**111. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ndio taasisi inayohusika moja kwa moja na maisha ya kila siku ya watanzania kwa ngazi zote. Kwa mwaka wa fedha 2016/17 taasisi hii ilikadiriwa kukusanya maduhuli yapatayo shilingi trilioni 16.881 na kati ya fedha hizo hadi mwezi Februari, 2017 ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 4.75 tu, sawa na 28%. Na ukiangalia fedha hizo zimetokana na marejesho ya mshahara, na kuuza vifaa chakavu na zabuni makao makuu. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema vyanzo hivi sio vyanzo vya uhakika kuweza kutegemewa na taasisi kubwa kama hii ya

Tamisemi inayogusa maisha ya watu ya kila siku. Kama mishahara isiporejeshwa na vyuma chakavu vikimalizika? Maana yake hakuna fedha zitakazopatikana!!!!!!!!!!.

**112. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi ya kawaida na maendeleo Tamisemi ilipangiwa kiasi cha shilingi bilioni 354.383 kati ya hizo shilingi bilioni 325.469 ni kwa ajili ya mpango wa maendeleo, ikiwa shilingi bilioni 256.739 zikiwa fedha za ndani na shilingi bilioni 68.730 zikiwa fedha za nje.

**113. Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa uwekezaji muhimu ni ule ambao utasaidia kuwa chanzo cha mapato kwa halmashauri, miradi ya ujenzi wa vituo vya mabasi 11, vituo 5 vya maegesho ya malori, machinjio 7 na masoko 9 katika miji 7 mradi huo haukupewa hata shilingi. Na miradi yenye muonekano wa kuwa vyanzo vya mapato kwa halmashauri ni mingi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kama kweli tunataka Serikali za mitaa kutimiza majukumu yao ni lazima miradi inayoweza kuwa vyanzo vya mapato itekelezwe kwa ukamilifu wake.

**114. Mheshimiwa Spika**, mpango wa utekelezaji miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/18 programu ya uendelezaji wa miji 18 kasma 6405 imetengewa shilingi bilioni 12.610 wakati mwaka jana walitengewa bilioni 10.47 na hakuna hata shilingi iliyotolewa, na mbaya sana ile miradi iliyotakiwa kutekelezwa mwaka jana, mwaka huu haipo kwenye program ya utekelezaji badala yake itatekelezwa mradi mipya, na fedha zote za program hii ni

kutoka nje. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kunakosekana umakini wa "consistence" katika upangaji na utekelezaji wa miradi yake. Kwa mwendo huu ni dhahiri hatuwezi kupiga hatua yoyote katika kuendeleza Halmashauri zetu.

## XXXI. HITIMISHO

**115. Mheshimiwa Spika,** katika kuhitimisha ni muhimu kuelewa kwa undani dhana ya **"all development are local",** katika muktadha wa halimashauri zetu pamoja na Serikali za mitaa katika kulete maendeleo kwa wananchi, na maendeleo ni lazima yawe kwa watu. Uelewa wa na ufahamu wa mahitaji ya mamlaka ya serikali za mitaa na jamii inayoishi hapo na kutoa msaada wa hali na mali ili kuwa na maendeleo shirikishi, ndio njia pekee itakayohakikisha jamii ya kitanzania inakuwa na maendeleo endelevu.

**116. Mheshimiwa Spika,** dhana ya **"all development are local"**,ni kwamba maendeleo endelevu yanapatikana kwa ushirikishwaji wa wananchi na sio kutokana na maelekezo na matamko ya viongozi na Serikali za mitaa ndiko wananchi walipo na sio Serikali kuu. Aidha tukumbuke kauli ya Mwalimu Nyerere kwamba; "Maendeleo ni ya watu na sio ya vitu". Ukweli ni kwamba sasa hivi maendeleo ni kwa vitu na jambo hilo wananchi wengi sasa hivi wanakula bombardier badala ya kula ugali na wali. "You cannot

develop people, you must allow people to develop themselves"

**117. Mheshimiwa Spika,** "THE 2030 AGENDA FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT" malengo ya Milenia mapya endelevu ya Umoja wa Mataifa hasa lengo la 16. Kuwa na maendeleo shirikishi kwa jamii, na haki kwa wote, na kujenga taasisi inayowajibika kwa ngazi zote.

> ***"Promote peaceful and inclusive societies for sustainable development, provide access to justice for all and build effective, accountable and inclusive institutions at all levels"***

Kama ambavyo alisema Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa ni lazima kuwepo na ushirikishaji wa jamii ambayo ndiyo injini ya uchumi wa nchi na jamii hiyo inaishi vijijini.

**118. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi inaitaka Serikali kuu, kama kweli inataka ustawi na maendeleo ya wananchi "economic Development" kuzirejeshea halmashauri zetu uhuru wa kuamua jinsi raslimali zake zitakavyotumika kama ambavyo lengo la maboresho ya Serikali za Mitaa (LGRP) lilivyokuwa likihitaji. Ila kama Serikali inahitaji "economic Growth" basi iendelee na utaratibu uliopo sasa.

**119. Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**……………………………………..**

**Japhary Raphael Michael (Mb)**

**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-**

**Ofisi ya Rais- TAMISEMI**

**18.04.2017**